**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MJI KIBAHA**

# SHULE YA SEKONDARI VIZIWAZIWA

**NAMBA ZA SIMU**
**Mkuu wa shule, 0768648807, 0783821757** **S.L.P 30112,**
**Makamu mkuu wa shule 0716551892,0769226874**
**KIBAHA-PWANI**

**Kumb.Na.VSS/……………………….**
**Tarehe …………….**
**Ndugu: ……………………………………………..**

**<u>TAARIFA YA KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO ………..</u>**

Ninayo furaha kukufahamisha kuwa umechaguliwa kuingia kidato cha Tano tahasusi ya …………. mwaka wa masomo wa ……………. Unatakiwa kufika hapa shuleni tarehe …………. Shule ya sekondari **VIZIWAZIWA** iko katika **Mkoa wa pwani, Halimashauri ya Mji Kibaha** kata ya **VIZIWAZIWA**, Mtaa wa **SAGALE KAMBINI** Umbali wa kilomita saba (07) kutoka kituo cha Daladala **KWAMFIPA** au **MSIKITINI** Barabara kuu ya Morogoro. Usafiri wa kukufikisha shuleni ni pikipiki ambazo zinagharama ya tsh 3500/=. Kila mwanafunzi atajitegemea kwa safari zote za kuja shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo au dharura yoyote ile.
Yafuatayo ni maelezo na maagizo ambayo unapaswa kuyazingatia kabla hujafika hapa shuleni.
TUNASISITIZA FOMU HII KURUDISHWA BILA KUPUNGUZWA KURASA YOYOTE, ni mategemeo yetu kuwa mtasoma (Mzazi/Mlezi na Mtoto) kwa makini na kuzielewa.

**1. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**:

i. Fika na Fomu ya kupimwa afya ikiwa imejazwa kikamilifu na Daktari wa Serikali.
ii. Leta File/Jalada la kutunzia mitihani yako.
iii. Fika shuleni ukiwa na kadi ya BIMA ya afya kama huna, piga simu shuleni kwa maelezo Zaidi namna yakupata bima ya afya
iv. Picha 3 passport size.

**2. SARE YA SHULE:**

- Suruali mbili za rangi ya **KIJANI JESHI** (Esteem No 1) zilizoshonwa na selebration (marinda mawili) yenye upana inch 14 na turn up, ziwe zimeshonwa kwa heshima na zisiwe za kubana(MODAL) kwa ajili ya darasani.
- Mashati mawili (MEUPE) ya mikono mirefu
- Tai ya (**KIJANI JESHI**) yenye michirizi myeupe{zinapatikana pia duka la shule}
- Fulana **KIJIVU MPAUKO** yenye kola na mfuko wa mbele (T-shirt) yenye nembo ya shule ambayo itatumika kama sare rasmi ya shule[zinapatikana duka la shule kwa anayehitaji]
- Suruali mbili za rangi ya DARK BLUE. kwa ajili ya kushindia na kazi za nje, haya ndio yatakuwa mavazi yake kipindi chote atakachokuwa shuleni, hataruhusiwa kuvaa nguo za nyumbani (unaweza kuja kushona shuleni).
- Fulana mbili za rangi ya BLUE BAHARI zenye kola na mfuko wa mbele na ziwe na nembo ya shule[Zinapatikana shuleni]

- SWETA moja ya **KIJANI JESHI yenye nembo ya shule** (Zinapatikana shuleni kwa anayehitaji)
- TRACKSUIT Moja ya KIJANI JESHI yenye nembo ya shule. (Zinapatikana shuleni kwa anayehitaji)

**MENGINEYO KUHUSU SARE YA SHULE**

i. Viatu jozi moja au zaidi visivyo chongoka wala kuinuka mbele. Hivi viwe vya ngozi rangi nyeusi (vyenye gidamu) vya kufungwa kwa kamba.
ii. Soksi fupi jozi mbili (au zaidi) za rangi nyeusi na zisizo na mapambo yoyote.
iii. Aje na mkanda mweusi wa ngozi wa suruali wenye "buckle" ndogo.
iv. Raba za michezo NYEUPE jozi moja(01)
v. Bukta mbili na jezi zake mbili za rangi ya kijani).
vi. Aje na kanda mbili pea moja.

**MAHITAJI MENGINE:**

(i) Kila mwanafunzi awe na Sahani, Bakuli, Kikombe, Kijiko kwa ajili ya chakula.
(ii) Alete Shuka tatu za Bluu, mto na Foronya mbili, pamoja na Chandarua.
(iii) Blanketi moja kama una changamoto ya afya.
(iv) Taulo moja ya kuogea na vifaa vingine vya usafi wa binafsi.
(v) Ndoo 3 za Lita 10 kwa ajili ya kutunzia maji ya kunywa na kuogea.
(vi) Jembe 1 lenye mpini na Mfagio laini1 (Soft broom) (kwa wanafunzi wa HGK)
(vii) Vyekeo au kwanja 1na Mfagio Mgumu 1(hardbroom) (kwa wanafunzi wa( PCM)
(viii) Dawa ya kusafishia choo Lita tano (AINAYA CARELINE) kwa wote [zinaweza pia kupatikana duka la shule]
(ix) Toilet Paper kumi (10) au zaidi kwa matumizi binafsi.
(x) Truncker imara la chuma na lenye kufuli.
(xi) Daftari kubwa 10 (counter books Quire 4) [zinaweza pia kupatikana duka la shule]
(xii) Ream" mbili za karatasi za "Photocopy" aina ya DOUBLE A (AA).[zinapatikana duka la shule]
(xiii) Scientific calculator 1.
(xiv) Jitahidi mnunulie mwanao vitabu vifuatavyo kwaajili ya rejea:-.
  - Physics Advanced Level by Chand, Chemistry Advanced level by Chand.
  - Modern ABC Physics volume1 and 2.
(xv) Mfungulie mwanao akaunti Benki kwa ajili ya kutunza fedha za matumizi.
(xvi) Aje na koti/ kanzu(Laboratory Coat) ya maabara nyeupe kwa ajili ya masomo ya Sayansi kwenye kazi za maabara isipokuwa tahasusi ya masomo ya sanaa
(xvii) Godoro moja lenye Futi 2½ kwa 6.

**3. MICHANGO**

**Michango ilipwe kwa utaratibu na viwango vilivyooelekezwa katika jedwali hapa chini.**

| SN | AINA YA MALIPO | KIASI(Tshs) | MAHALI PA KULIPIA |
|---|---|---|---|
| **1.** | Uendeshaji wa shule | 65,000 | **LIPA KWENYE AKAUNT YA CRDB NA:0150720115100 JINA: VIZIWAZIWA SECONDARY.** ***Unapolipa andika jina kamili la mwanafunzi.*** |
| **2.** | Nembo ya Shule | 5,000 | |
| **4.** | Picha na Kitambulisho | 5,000 | |
| **5.** | Tahadhari | 5,000 | |
| | **JUMLA KUU** | **80,000/=** | |

NB: Unaporipoti shuleni njoo na risiti za benki.**HAKUNA HELA ITAKAYOPOKELEWA MKONONI.**

## 4. MAELEKEZO MENGINE MUHIMU:

(i) Usafiri wa kurudi nyumbani wakati wa likizo unaratibiwa na uongozi wa shule, hivyo mzazi/mlezi utawajibika kutuma nauli wiki mbili kabla ya shule kufungwa.

(ii) Utakapofika hapa shuleni utasomewa sheria za shule na utaratibu mzima wa shule hii na utalazimika kuufuata. Ukikosa, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yako.

(iii) Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki Simu,line ya simu au kuwa na vocha za simu, redio pasi , Laptop , "Ipad" au kifaa chochote kinachotumia umeme au kuwezesha mawasiliano kinyume na taratibu shuleni. Akipatikana na vitu hivyo, atafukuzwa shule.

(iv) Endapo mwanafunzi/mzazi/mlezi utakuwa na dharura wasiliana na uongozi wa shule kwa kutumia namba zifuatazo:

**Mkuu wa shule, 0768648807, 0783821757**
**Makamu mkuu wa shule 0716551892,0769226874**

## 5. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULENI.

(i) Kumiliki simu ya mkononi, laini, chaja ya simu au kifaa chochote kinachotumia umeme na kusaidia mawasiliano kutumia simu isiyotambuliwa na shule shuleni.
(ii) Wizi,
(iii) Uasherati na ubakaji
**(iv) USHOGA.**
(v) Ulevi, uvutaji bangi na matumizi ya madawa ya kulevya.
(vi) Makosa ya jinai.
(vii) Kupigana au kupiga
(viii) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
(ix) Kudharau Bendera ya Taifa.
(x) Kuoa
(xi) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule.
(xii) Kukataa adhabu.
(xiii) Kutoroka na kulala nje ya shule bila ruhusa
(xiv) Kufanya udanganyifu kwenye mitihani ya ndani na nje.
(xv) Kuficha uovu /uhalifu /mhalifu
(xvi) Kukaribisha wageni ndani ya shule bila ruhusa ya Mkuu wa shule

## 6. KIKAO CHA WAZAZI

Shule ina utaratibu wa vikao vya wazazi ambavyo hufanyika kila mwaka.Lengo kuu la vikao hivyo ni kupanga na kusimamia mipango mbalimbali ya kuboresha taaluma,nidhamu na miundo mbinu ya shule. Mwaka huu kikao kitafanyika tarehe **04/09/2026** kuanzia saa tatu kamili asubuhi. Karibuni sana.

**7. HITIMISHO**

Mwisho natumia fursa hii kwa niaba ya walimu, wafanyakazi na wanafunzi wote wa shule hii kukukaribisha hapa shuleni. Karibu sana.

Abasi Ramadhani Kiwayo
Mkuu wa Shule,
**SHULEYA SEKONDARI VIZIWAZIWA.**
**SIMUYAMKONONI: 0768648807**

For: THE HEAD MASTER
VIZIWAZIWA SECONDARY SCHOOL
P.O. Box 3011[illegible]
KIBAHA-PWANI

**TAARIFA YA MWANAFUNZI**

**Anuani……………………**

**Tarehe:..........................**

**Mkuu wa Shule,**
Shule ya Sekondari Viziwaziwa,
S.L.P 30112,
**KIBAHA**

**YAH: BARUA YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE**

Asante kwa barua yako Kumb. Na…………………………….. ya tarehe……………………

a) Nakubali/sikubali nafasi niliyopewa ya Kidato cha Tano kwa mwaka……………………………………………
b) Niko tayari / siko tayari kufuata sheria, maagizo na masharti yote ya Viziwaziwa Sekondari
c) Nitahudhuria/Sitahudhuria masomo yote ninayotakiwa kusoma hapa shuleni
d) Nikishindwa kuhudhuria bila sababu ya msingi nifukuzwe shule.
e) Nitaleta / Sitaleta
   (i) Uthibitisho wa Uraia / Cheti cha kuzaliwa (Affidavit hairuhusiwi)
   (ii) Vitu vinavyohitajika kwa matumizi yangu
   (iii) Cheti cha Afya
   (iv) Fomu ya kuandikisha na habari zangu za mzazi / mlezi wangu.
   (v) "Result slip" ya kidato cha nne.

Asante

………............................................................ ………………………………..

**JINA LA MWANAFUNZI** **SAINI YA MWANAFUNZI**

## FOMU YA KUANDIKISHA SHULENI NA HABARI ZA WAZAZI WA MWANAFUNZI

### SEHEMU A: (HABARI ZA MWANAFUNZI):

1. Jina kamili (Kama kwenye mtihani)……………………………………………………………….
2. Tarehe ya kuzaliwa……………………Dini……………………..Dhehebu……………………
3. Mahali na Wilaya ulipozaliwa………………………………………………...………………
4. Shule ulipomaliza Kidato cha IV………………………………… Mwaka uliomaliza………
5. Kidato unachokuja kuingia hapa shule ya Sekondari ya Kibaha……………………………...
6. Namba yako ya mtihani wa Kidato cha Nne …………………………………..…………….
7. Michezo unayopendelea:

| S/N | JINA LA MCHEZO |
|---|---|
| 1 | |
| 2 | |
| 3 | |

8. Kazi yeyote ya uongozi uliyowahi kufanya kamavile kiongozi wamichezo, kwaya, ngoma, kiranja, maktaba n.k.

| MADARAKA (UONGOZI) | SHULE/MAHALI | MWAKA |
|---|---|---|
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |

9. Mambo unayopendelea kufanya nje yamasomo (kama vile michezo, mpira, bustani, ushonaji viatu, nguo,ujenzi, kuchomelea, michezo ya kuigiza kuimba)

   1………………………………….2……………………………….3…………………….

10. Ndugu wa karibu wa mwanafunzi (wa kiume/ wakike) kama, vile mjomba, mama, baba, shangazi, kaka, dada kufuatana na umri wao wa kuzaliwa.

| S/N | JINA LA NDUGU | KAZI ANAYOFANYA | UHUSIANO NA MWANAFUNZI | KIWANGO CHA ELIMU | ANUANI | NAMBA YA SIMU |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **1.** | | | | | | |
| **2.** | | | | | | |
| **3.** | | | | | | |
| **4.** | | | | | | |
| **5.** | | | | | | |

**PICHA ZA WAZAZI NA NDUGU WENGINE WENYE MAJINA KWENYE JEDWALI, ZIBANDIKWE KWA MFUATANO HAPA CHINI KWA JINSI MAJINA YALIVYOANDIKWA.**

**1** **2** **3**

**4** **5**

Nathibitisha kwamba habari zilizo tolewa hapo juu ni kweli. Naahidi kuwa natabia nzuri, mchapakazi na mwenye bidii ya masomo.

**Tarehe:**…………………………..**Saini ya Mwanafunzi**……………………….……….

**TANBIHI**:
**Hairuhusiwi kubadili dini ukiwa shuleni au kushawishi wanafunzi wengine kubadili dini**.

**SEHEMU B: (HABARI ZA MZAZI/MLEZI)**:

1. Jina kamili………………………………………………………………………………

2. Kazi yake.………………………………………………………………………………

3. Mahali anapoishi……………………………………………….

Anwani ya nyumbani

Barabara…………………Kijiji/Mtaa……………………...Kata…………………Tarafa………

Wilaya………………….Mkoa…………………

4. (a) Anwani ya Mahali pa kazi ya mzazi / mlezi…………………………………………….

(b) Nambari ya simu………………………..Namba ya nyumba…………………….

5. Dini ya mzazi……………………………..dhehebu…………………………………………

6. Anuani kamili ya nyumbani ambako mtoto atakuwa ana kwenda siku za likizo.………………………………………………………………………………………

7. Anwani ya kazini (ikiwa inatofautiana na hiyo hapo juu na kila mara inapobadilika tunaomba utuarifu rasmi kwa barua) ……………………………………………………………………

8. Nathibitisha kwamba habari zilizo tolewa hapo juu ni za kweli.

9. Naahidi kushirikiana na walimu kuhakikisha kwamba kijana wangu anakuwa na tabia nzuri, mchapakazi na mwenye bidii ya masomo.

**Saini ya Mzazi/Mlezi**…………………………………**Tarehe………………………..**

**MINISTRY OF EDUCATION SCIENCE AND TECHNOLOGY**
**VIZIWAZIWA SECONDARY SCHOOL**
**P.O BOX 30053, KIBAHA**

## SPECIAL REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

The Medical Officer………………………………….From Headmaster, (GOVERNMENT M.O) Kibaha Secondary School, Date:………………………Name of Student……………………………….............Date…………………Term …..…… Year……………..I shall be very grateful if you will kindly examine the above named student and give us a report regarding his fitness to undertake studies well in our school.

A: **PRELIMINARY INFORMATION: MEDICAL HISTORY**

| S/N | DISEASE | YES | NO | | DISEASE | YES | NO | | DISEASE | YES | NO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Tuberculosis | | | 7 | Kidney/trouble | | | 13 | Operation | | |
| 2 | Asthma | | | 8 | Diabetes | | | 14 | Eye disorder | | |
| 3 | Pneumonia | | | 9 | Nervous breakdown | | | 14 | V.D | | |
| 4 | Heart trouble | | | 10 | Ear/Noise/throat trouble | | | 16 | Disabled | | |
| 5 | Recurrent digestion | | | 11 | Skin disorder/ Disease | | | 17 | | | |
| 6 | Jaundice | | | 12 | Anaemia | | | 18 | | | |

**B: VITAL STATISTICS**

Age………………..Height………………Weight……………..Blood group…………
Blood pressure………………………. Pulse rate…………………………..
Systolic………………………………… Diastolic…………………………….

**C: MEDICALEXAMINATION:**

| | **REMARKS/TREATMENT** |
|---|---|
| EAR | RT LT |
| VISION | RT.EYE LT.EYE |
| CHESTEXAMINATION | |
| ABDOMINALEXAM | LIVER SPLEEN |
| | OTHER COMMENTS |
| M.S.SYSTEM | UPPER LIMB |
| | LOWER LIMBS |
| | SKIN |
| ANYOTHERFINDING | |

**D: LABORATORY EXAMINATIONS/INVESTIGATION:**

(1) STOOL: - Ova………………………..Leucocytes…………………
(2) URINALYSIS:
PROTEIN…………………………………GLUCOSE…………………SEDMENT:-
OVA……………………Leucocytes……………………
(3) Hb…………………………………………………………………………………….
(4) B/S……………………………………………………………………………………
(5) VDRL…………………………………………………………………………………
(6) WBC Total………………………………………………
Differential: N……L…M…E…B………..
(7) X-ray Chest (If necessary)…………………………………………………….
(8) ANY OTHER INVESTIGATION…………………………………………

**MEDICAL CERTIFICATE:**

We request the medical officer to complete the following:

I have examined the above named student and considered that is physically fit/ unfit for most activities taken at the school as my findings indicated above.
**Date**:……………… **Station**…………………..**Dr'sName**:……………… **Signature**……………

Mwisho natumia fursa hii kwa niaba ya walimu, wafanyakazi na wanafunzi wote wa shule hii kukukaribisha hapa shuleni. Karibu sana.

Abasi Ramadhani Kiwayo
Mkuu wa Shule,
**SHULEYA SEKONDARI VIZIWAZIWA.**

Ref: THE HEAD MASTER
VIZIWAZIWA SECONDARY SCHOOL
P.O. Box 3011?
KIBAHA-PWANI